HUKMU YA HEDHI NA NIFASI



NA

YANAYOFUNGAMANA NAYO KATIKA HUKMU ZA KISHERIA

MASJID AL-FAROUQ

MKELE - ZANZIBAR

UTANGULIZI

Hakika sifa njema anastahiki Allah . Tunamuhimidi na tunamuomba na tunamtaka msamaha na tunamtaka uongofu na tunajikinga kwake kutokana na uovu wa nafsi zetu na ubaya wa matendo yetu, anayemuongoza Allah hakuna wa kumpotosha na anayemuacha Allah apotee hakuna wa kumuongoza.

Ama baada ya hayo, hii ni risala fupi sana iliyosheheni yote yanayofungamana na mwanamke mwenye hedhi na nifasi katika hukmu za kisheria, tumeiandaa risala hii kutokana na haja ya wengi katika hili, na kutokana na kujiweka mbali mno Wanawake na suala zima la kusoma dini yao. Wengi katika wanawake leo wanateseka na kutaabika hadi kuyumbishwa katika mas-ala haya ya Hedhi na Nifasi ukiachilia mambo mengine katika dini yao.

Kwa kuelewa wito wa mas-ala haya na Ikhtilafu ziliopo baina ya wanachuoni, tumejitahidi kunakili kauli za wanachuoni zilizoshiba hoja kutoka katika Qur-an na Sunna kwa ufahamu wa wema waliotangulia. Hivyo, utaona ndani ya risala hii tumezipitia kauli za wanachuoni zilizoegemea katika Kitabu na Sunna na tumejiepusha na utaasubi (uhafidhina) na kun'gan'gania rai ya Fulani pasi na Fulani.

Tunatarajia Allah atawanufaisha Wanawake wengi kwa risala hii fupi sana pamoja na Waislam mbali mbali pamoja na kufanyia kazi walichokisoma, bila ya kusahau Ikhlasi juu ya jambo hili, pia huenda wakastaajabu na yale yaliyomo ndani ya risala hii kutokana na mazowea ya waliyokua nayo, lakini tunasisitiza na kuelekeza nasaha zetu ni kuangali jee wapi dalili ilipoegemezwa, elewa ni kitabu (Qur-an) na Sunna kwa ufahamu wa wema waliotangulia.

بسم الله الرّحمن الرّحيم

HEDHI

Kilugha ni mchuruziko.
Kisheria ni damu ya kimaumbile inayomtoka mwanamke katika masiku maalumu. Allah, amefanya kwa rehma zake na hekma zake ni katika uzazi wa mwanamke, pia ni chakula cha mtoto aliyetumboni na kwa maana hiyo mwenye mimba hapati hedhi na kwasababu damu hii kwa idhini ya Mola inamuendea mtoto aliyetumboni kwa kupitia kitovuni kujitawanya katika mishipa kwa kumpa nguvu, kwa kua mtoto haiwezekani kula wala kunywa ndani ya tumbo la mama yake, kwani lau atakula na kunywa litahitaji jambo hilo kuyatoa yale mabaki.
Hedhi ni damu ya kimaumbile sio damu inayozuka tu au kutokea kwa jambo Fulani bali ni katika maumbile ya Mwanadamu, kinyume na damu ya **ISTIHADHA** kama tutakavyoeleza inshaallah, bali ipo hadithi sahihi inayotia nguvu kauli hii {..... katika hiyo hedhi ameifaradhisha Allah kwa watoto wa kike wa Adam} Alhadithi angali Bukhari (303) na Muslim (1211). Yaani Mola amemuandikia Mwanamke kwa kumkadiria. Pia imepokewa kuwa wanawake wawili katika tarekhe Mola hakuwapa na kuwateremshia damu ya hedhi katika maisha yao. Bi Maryam na Fatma bint Muhammad.

WAKATI WAKE:

Wengi katika wanachuoni wanaona kwamba wakati ni baada ya mtoto wa kike kufikia miaka {9} ambapo ni miaka ya Qamariyya yaani idadi ya masiku ya mwezi muandamo sio masiku ya jua kwa maana hiyo hapana hedhi ya kisheria kabla ya miaka tisa, hivyo

atakapopata mwanamke hedhi kabla ya kufikia miaka tisa hiyo siyo hedhi, hata kama itaingia hedhi katika njia inayofahamika na kwa ile damu inayofahamika basi hiyo haitokua ni hedhi bali ni mshipa wa damu na hivyo hazitomthibitikia juu yake hukmu za mwenye Hedhi, na huenda ukarefuka muda wa kukomea na kwisha kwake , kwahivyo mwisho wa kwisha kwake ni mwisho wa umri wake. Amesema Ibnu Taymiyyah kwamba "haikusihi kuweka mpaka wa siku na wakati utakapoona damu ijuulikanayo na wanawake basi hiyo ni Hedhi. Hivyo basi wakati wowote kikongwe akiona damu basi hiyo ni Hedhi.

- **RANGI YAKE:** Inashurutishwa damu ya hedhi iwe na moja hali ya rangi zifuatazo:
- **NYEUSI:** Kutoka kwa Fatma bint Abii Hubayah, hakika yake alikua ni mwenye kuendelea kutokwa na damu ya Hedhi, Mtume {Swallallahu a'layhi wasallam} akamwambia "Ikiwa kama ni damu ya hedhi basi ni nyeusi inayojuulikana , basi ikiwa kama hivyo jizuwie na sala na pia ikiwa nyengine basi hapo tawadha na usali".
  Ameitoa Abuu Daudi No. 304 na Nasaii No. 216 na Ibnu Hibbaan Juz 4 uk 180.
- **UWEKUNDU:** Kwasababu hiyo ni asili ya rangi ya damu.
- **UMANJANO:** Nao ni ule umanjano anaouona kama usaha unaelea juu yake umanjano.
- **UCHAFU:** Nao ni ukati na kati baina ya rangi nyeupe na nyeusi kama uchafu. Kutoka kwa Alqama bi abii Alqama amepokea kutoka kwa mama yake amesema "Walikua wanawake wakimpelekea Bi Aisha Dirja {chombo anachoweka mwanamke manukato yake na Mapambo} mkiwa na pamba na umanjano , basi Bi Aisha husema, "Msifanye haraka mpaka muione pamba iko

safi {nyeupe}" ameitoa Imamu Baihaqiy Juz 1 uk 336 pia angalia Irwaul- ghalili Juz 1 uk 218 na inazingatiwa umanjano na uchafu kuwa ni hedhi katika wakati wa siku za hedhi na nje ya kipindi hicho haitozingatiwa kuwa ni hedhi dalili kutoka kwa Ummu A'twiyyah {R.A} amesema: "tulikua hatuzingatii umanjano na uchafu baada ya tohara kuwa chochote" ameitoa Abuu Daud 307 Nassaiy Juz 1 uk 187.

- **MUDA WAKE:** Haikadiriki hedhi katika uchache na wingi wa muda wake na wala haikuja dalili ya wazi katika kuweka mpaka wa muda wake na huu ndio msimamo wa Shekhul- Islam Ibnu Taymiyyah. Pia kuna wengine wakaegemea katika desturi kwa kusema uchache wake ni mchana mmoja na usiku. Hivyo lau kama mwanamke ataona damu kwa muda wa masaa ishirini hata kama ikiwa ni harufu yake, rangi yake, kwani itayopungua chini ya mchana na usiku mmoja siyo hedhi, lakini hili halina dalili ndani yake kwani wapo wanawake wasio na hedhi, na wengine hupata hedhi muda mchache kisha hutoharika.

Pia wengine wakaegemea katika desturi kwa kuweka mpaka wa siku kumi na tano {15} ni wingi wake, kwa kudai itakayozidi zaidi ya muda huu ni kuzama ndani ya muda mwingi na kila kilichi kingi kinathibiti kwake hukmu ya yote, lakini haya tunasema hayana dalili na lau kama wangeegemea katika dalili juu ya madai haya waliyoyasema tungelikubali na kuyapokea, hivyo kwa mfano ikiwa kwa mwanamke kuna desturi ya siku kumi na saba {17} zilizodumu tunasema, zote hizo ni siku za Hedhi. Ama kama itaendelea damu kila mwezi yaani mwezi mzima au kukatika muda mchache kama siku moja au mbili ikiwa inakuja kwa kukatika katika kwa nyakati tofauti na kutoweka katika mwezi baadhi ya saa, Mwanamke huyu atakua ni "Mustahadha".

Lakini desturi yake hiyo hedhi ni siku sita na hili ni sahihi kwa kuthibitisha kauli yake { Swallallahu a'layhi wasallam} kumwambia Yule mwanamke mwenye Istihadha "…….. Kuwa katika hedhi ndani ya elimu ya Allah kwa muda wa siku sita au saba……." ameitoa Bukhari {227} na Muslim {262}. Na hili ni katika uhalisi kwani wengi katika wanawake wapo katika sita au saba.

MUDA BAINA YA TOHARA MBILI ZA HEDHI:

Wameafikiana maulamaa ya kwamba hamna mpaka kwa wingi wa tohara muda uliopo baina ya Hedhi mbili na wakatafutiana katika uchache wake. Wakasema baadhi yao siku kumi na tatu {13} hivyo wakasema lau mwanamke akitoharika kutoka katika hedhi yake na baada ya siku kumi na mbili ikaingia damu, hii siyo hedhi kwasababu uchache wa tohara baina ya tohara mbili ni siku kumi na tatu.

Bali utasema haikuja dalili inayoweza kusimama kwa kutolea hoja juu ya uchache wa muda wa hedhi baina ya tohara mbili.

FAIDA

- Pindi atakapoona mwanamke ameshatoharika na akakosa maji maji ya kujitoharishia kwa hakika atayammam na inajuzu kufanya tendo la ndoa. Angalia sahihi ……. Sunna Juz 1 uk {207} na ndio kauli ya wengi katika **Ahlul-ilmi.**

ISTIHADHA

Ni hali ya kuendelea kuchuruzika damu na kutoka kwake katika wakati usio wa hedhi na nifasi au ikaingia na yote mawili (Hedhi na Nifasi) hii ni damu isiyo ya desturi wala maumbile bali ni mshipa au shetani.

HALI ZA MUSTAHADHA

Mustahadha ana hali tatu kuu zenye kujuulikana, nazo ni :-

1. Inakua muda wa hedhi ni wenye kufahamika kwake kabla ya kupata jambo hilo, na katika hali kama hii atazingatia muda ule ujuulikanao ndio muda wa hedhi na kinachozidi katika hedhi yake itakua ni Istihadha na wala sio damu ya hedhi. Amesema Mtume {Swallallahu a'layhi wasallam} kumwambia mwanamke (…….. kaa kiwango cha ilivyokua ikizuwia hedhi kisha koga na usali) ameitoa Muslim {264} Abuu Daudi {279} na Imamu Naassaiy Juz 1 uk {119}.
2. Inakuwa ni kuendelea kutokwa na damu na wala haik…… masiku yenye kueleweka. Ama amezisahau siku zake amebaleghe moja kwa moja kama ni Mustahadha na wala hawezi kupambanua baina ya damu ya Hedhi na nyengine, katika hali hii itakua hedhi yake ni siku sita au saba. Na ikiwa sababu ya wingi wa ada ya wanawake waliomzunguka baadae atakoga na wala haitozingatiwa damu baada yake kwa…. hiyo ni "Istihadha". Yamekuja mafunzo ya Mtume kwamba, alimwambia Lohmmat bint Jahsh "nitakuamrisha mambo mawili, lolote ulifanyalo limejitosheleza na jengine hu…… msukumo katika misukumo ya shetani, basi kuwa mwenye hedhi siku sita au saba katika ilimu ya Allah, kasha koga mpaka utakpoona umetoharika na ukasafishika

basi Sali siku 24 au 23 na ufunge kwani hilo litakutosha, basi fanya hivyo kadhalika katika kila mwezi, kama wanavyokua katika hedhi wanawake na kama wanavyojitoharisha kwa nyakati za hedhi zao kwa ajili ya tohara, na kama ikikuwiya uzito (jambo jengine la kufanya, zicheleweshe Adhuhuri na uharakize Laasiri basi ukoge Alhadath. Amesimulia Abuu Daudi {287} Ibn Mjjah {622}

3. Hana mwanamke desturi (ada) lakini ana uwezo wa kupambanua na damu ya hedhi na ile isiyo ya hedhi katika hali hii atafata upambanuzi, ataangalia damu yake tu ikiwa ni ya hedhi, ataanza kusali na kama ni nyengine atasali kwa dalili ya hadithi:- Fatma bint Hubayshi, Hakika yeye alikua Mustahadha (anaendelea kutokwa na damu) Mtume { Swallallahu a'layhi wasallam} akamwambia "Pindi ikiwa damu ya hedhi huwa ni nyeusi inayofahamika ikiwa katika hali hiyo jizuwie na sala na ikiwa ni nyengine basi tawadha na usali, si vyenginevyo huo ni mshipa, amitoa Bukhari (228) Muslim (262).

HUKMU ZA MUSTAHADHA

1. Si lazima juu yake kukoga katika kila kipindi cha sala ispokua mara moja tu pale inapokatika hedhi yake.
2. Inafaa kwa mumewe kufanya tendo la ndoa pamoja hali ya kutokwa na damu.
3. Inafaa kukaa msikitini, kushika msahafu, kusali na kufanya kila aina ya ibada.
4. Ama suala la kutawadha kwa Mustahadha katika kila kipindi cha sala anapotaka kusali, hakika wamekhitilafiana wanavyuoni, wapo walosema: lazima kutawadha katika kila sala kama Imamu Shafi, Imamu Albani nk. Angalia Thamarul mustataba Juz 1 uk {41} pia kwa kauli hii amesema Sheikh Said Sabiq katika Fiqhi

sunna Juz 1 uk {66} na wapo walosema sio wajibu kutawadha katika kila sala bali inapendezeshwa tu jambo hilo kama alivyokwenda nalo Sheikh Abuu Malik Kamaal Said Salum. Angalia Sahihi fiqhi Sunnah Juz 1 UK (217) pia angalia Jaamii Ahkamu Nissai Juz 1 uk (230).

MAMBO YALIYOHARAMU KWA MWENYE HEDHI NA NIFASI

1. **SALA**

Wamekusanya tamko la pamoja wanavyuoni juu ya uharamu wa sala kwa wenye hedhi na nifasi, ikiwa sala ya faradhi au sala ya sunnah na itakua imemuondokea dhima ya jambo hilo kipindi chote cha jambo moja kati ya hayo mawili. Hivyo haitomuwajibikia kuja kuzilipa baada ya kutoharika. Kutoka kwa Abuu Said amesema "Amesema Mjumbe { Swallallahu a'layhi wasallam} ……..hivi haikuwa anapopata hedhi mwanamke huwa hasali wala hafungi basi huo ni upungufu wa dini yake" ameitoa Bukhari (1951) na Muslim (80) pia kutoka kwa muadh kwamba mwanamke mmoja alimwambia bibi Aisha "Jee atalipa mmoja wetu sala yake atapotoharika? Akasema jee wewe ni Hururiya (sifa ya mwenye kuitakidi ya Mkhawariji walikuwa baadhi yao wakiwajibisha kulipa sala kwa mwenye hedhi) akaendelea kusema tulikuwa tunapata hedhi wakati wa Mtume
{Swallallahu a'layhi wasallam} na wala hatuamrishi hilo au alisema hatulifanyi hilo) ameitoa Bukhari (321) na Muslim (265).

FAIDA

- Akipata hedhi mwanamke muda mchache kabla laasiri mfano na wala hakusali adhuhuri, je itamlazimu kulipa adhuhuri atapotoharika? Kauli yenye nguvu ni kuwa "hatolipa" kwasababu

wanawake zama za Mtume walikuwa wakipata hedhi katika nyakati zote na haik…….. Mtume { Swallallahu a'layhi wasallam} aliwaamrisha wao walipe sala baada ya tohara kwa zile sala zilizompita, amesema Sheikh Islam (……..na lililowazi zaidi katika dalili …... yeye haitomlazimu kitu……) angalia Fatawa Juz 23 uk {235}.

- Atakapotoharika mwenye hedhi muda mchache kabla ya sala ya laasiri kwa mfano. Basi pale atakapokoga tu ukaingia wakati wa sala ya laasiri, je itamlazimu kusali adhuhuri? "Amesema Sheikh Islam katika "Fatawa" juz 2 uk {3…} itamlazimu pindi tu akitoharika kutoka katika hedhi au nifasi kabla ya kuzama kwa jua asali adhuhuri na laasiri ya mchana huu na hivyo hivyo ikiwa atatoharika kabla kuchomoza Alfajiri itamlazimu kusali Magharibi pamoja na Ishaa katika usiku huu, kwasababu wakati wa sala ya pili ndio wa sala ya mwanzo katika hali ya adhuhuri. Pia angalia sahihi Fiqhi Sunnah Juz 1 uk {210}.

2. **FUNGA**

   Haifai kwa mwenye hedhi na nifasi kufunga, hata kama atafunga haitosihi funga yake na itakua ni batili ni wajibu juu yake kulipa zote zilizompita, katika masiku ya hedhi au nifasi katika mwezi wa Ramadhani, kinyume na zile zilizompita katika sala, hii ni kutokana na kuwa funga hai…. Katika mwaka ila mara moja tu, ama sala hujirejea mara nyingi. Basi kuwajibishwa funga juu yake ni jambo la wepesi sana, amesema Bibi Aisha (R.A) "Ilikua anatupa sisi ……. (hedhi) na tunaamrishwa kulipa funga na wala hatuamrishwi kulipa sala" ameitoa Muslim {265} na Abuu Daudi {263}.

FAIDA

- **Akitoharika mwenye hedhi kabla ya alfajiri na wala hajakoga, je! Atafunga siku hiyo?** Jawabu "Hakika mwenye

Hedhi akitoharika kabla ya alfajiri amekusudia (amenuwilia) funga yake, itasihi kufunga kwake na wala haitoegemea funga kusihi juu ya kukoga kinyume na sala.

- **Atakapotoharika mwenye hedhi kabla ya kuzama jua, je! Atafunga mchana uliobakia?** Jawabu "Haitomlazimu kujizuia baki ya mchana kwani yeye amekula katika mwanzo wake na atakuja ilipa siku hii m'badala wake, hivyo hakuna haja ya kujizuwia kwake.
- **Je! Inajuzu kufunga sita za Shawwal kabla ya funga ya kulipa Ramadhani?** Jawabu "Kufunga sita ndani ya Shawwal hazipatikani thawabu zake ila itakapokua amekamilisha mtu kufunga mwezi wote wa Ramadhani. Hivyo Yule ambae juu yake kuna deni la Ramadhani mtu huyo hatofunga sita za Shawwal ila baada ya kulipa Ramadhani, kwa kua Mtume { Swallallahu a'layhi wasallam} amesema "Yeyote atakaefunga Ramadhani kisha akafuatanisha sita za Shawwal …….) ameitoa Imamu Muslim {1164} Abu Daudi {2433} Tirmidhiy {759} Ibn Maajah {1716}. Kwa maelezo zaidi ya hili, rejea katika kitabu cha Sheikh Uthaymin Mumtaa Juz 6 uk {448}. Na juu ya hili tunasema kwa Yule mwenye deni ndani ya Ramadhani itakuwa uzuri kwanza kulipa madeni kisha atafunga funga sita za Shawwal.

3. **JIMAI {KUINGILIA}**

Kumuingilia mwenye hedhi haijuzu kwa makubaliano ya Maimamu wote kama alivyoharamisha Allah (S.W) hilo kwa kauli yake katika Qur-an

"Basi jitengeni na wanawake katika hedhi" {2:222}

Na amesema Mtume {Swallallahu a'layhi wasallam} "Fanyeni kila kitu ila Tendo la ndoa" Muslim {302} Na amesema Sheikh Islam: "Na kumuingilia mwenye Nifasi ni kama kumuingilia mwenye

hedhi, Haramu kwa makubaliano ya wanavyuoni" angalia Fatawa Juz 21 uk {624}.

FAIDA

- Kama ataitakidi Muislam uhalali wa jimai kwa mwenye hedhi atakua kafiri (amertadi), na kama atafanya hivyo bila ya kuitakidi hivyo kwa kusahau au kutojua kuwepo kwa hedhi au kutojua uharamu wake au kwa kulazimishwa, hapana makosa juu yake wala kafara. Na kama atamuingilia kwa makusudi kwa kujua kuwepo kwa hedhi na uharamu wake tena mwenye kulichagua jambo hilo kwahakika atakua amevamia maasi na atawajibika alete toba. Swali: Je! Atatoa kafara au hatotowa? Suala hili wamekhitilafiana wanavyuoni juu ya kafara ya mwenye kufanya jimai na mwanamke mwenye hedhi, wapo waloenda kwa kusema "Anatakiwa atowe fidia dinari moja au nusu dinari" angalia ……. Niylil Awtaari ya Imamu Shawkhani Juz 1 uk {244} dalili waliyoitumia ni ile hadithi ya Abuu Abaas kutoka kwa Mtume { Swallallahu a'layhi wasallam} juu ya Yule ambae amemuendea mkewe na hali ya kuwa yupo katika hedhi hakika amesema "atatowa sadaqa kwa dinari au nusu dinari" ameitowa Abuu Daudi {263} Ibnu Maajah {640} An-Nasaaiy Juz 1 uk {153}. (Kauli yenye nguvu juu ya hadithi hii ni dhaifu, na pia wapo walosema haitomlazimu kutoa kafara bali atatakiwa atubie kwa kule kufanya maasi na dalili walioitegemea ni hadithi hii hii lakini kwao wao wameidhoofisha. Angalia sahihi Fuqhi sunna Juz 1 uk {211-212} kwa ufupi dalili inayoonesha kuwa hapana kafara ndiyo yenye nguvu zaidi, na Allah {S.A} ndiye ajuae zaidi.
- Kinachokatazwa katika starehe kwa mwenye hedhi ni utupu "sehemu ya siri", mume ana haki ya kustarehe na mkewe mwenye hedhi kila kitu ispokua kuingiza katika utupu tu kwa dalili ya aya

na hadithi zilizotangulia zenye kuharamisha jimai wakati wa hedhi. Na kutoka kwa mmoja wa wakeze Mtume { Swallallahu a'layhi wasallam} "alikuwa Mtume {Swallallahu a'layhi wasallam} anapotaka kwa mwenye hedhi kitu, huweka katika utupu wake (mkewe) nguo" angalia Abuu Daudi {272} na dalili nyengine ipo pia kauli nyengine kwa wanavyuoni kwamba kinachojuzu kwa mwanamme ni kustarehe na mkewe sehemu zote ila kilichopo baina ya magoti na kitovu, nah ii ni kauli ya wanavyuoni wengi, inayo dalili zake lakini kauli ya mwanzo ni yenye nguvu zaidi kuliko hii.

4. **TAWAFU**

Nalo jambo hili ni haramu kwa mwenye hedhi kwa makubaliano, hii ni kutokana na hadithi ya Bibi Aisha, alipoingia katika hedhi wakati alikuwa ni hujaji alimwambia Mtume "Fanya kila anachokifanya hujaji ila usitufu nyumba (alkaba) mpaka utoharike" ameitoa Bukhari {1650}.

﴿ واالله أعلم﴾

YANAYOFAA AMBAYO NI HALALI KWA MWENYE HEDHI NA MWENYE NIFASI

❖ **KUGUSA MSAHAFU NA KUSOMA QUR-AN**

Na wala hatutambui dalili yoyote iliyowazi inayomzuwia mwanamke kugusa msahafu, hata hata ikiwa wanavyuoni baadhi wamekwenda kuwa mwenye hedhi haifai kugusa msahafu lakini wameshindwa kutoa dalili zenye kukubalika kuonyesha kuwa

jambo hilo halifai ndio maana akasema Ibnu Hazmi "kisomo cha Qur-an na kusujudu ndani yake na kugusa msahafu na kumtaja Allah (S.A) ni vitendo vya kheri inatakikana juu yake ni mwenye kulipwa mfanyaji wake, kwahivyo mwenye kudai limezuiliwa jambo hilo kwa baadhi ya hali Fulani, patalazimishwa juu yake kuleta dalili" angalia mahali Juz 1 uk {77-78}.

Pia suala la kusoma Qur-an mwanamke mwenye hedhi pamoja na nifasi wametofautiana wanavyuoni juu ya usahihi wake, basi amekwenda Imam Malik na shafii na kikundi cha wanavyuoni ya kwamba haifai kwa mwenye hadath kushika msahafu pamoja na kusoma na wakaegemea dalili katika mambo mawili:-

a. Kauli yake Allah "Hawaigusi hiyo ila wale waliotaharishwa" {Waqiah: 79}
b. Na hadithi ya Amru Ibn Hazmi ya kwamba Mtume { Swallallahu a'layhi wasallam} aliwaandikia watu wa Yemen barua na ndani yake kuna maneno "Asiiguse Qur-an ila aliyetohara"

Tunajibu madai hayo Kama ifuatavyo:-

a. Ama aya hii tukufu haiwezi kutegemewa kama ni dalili ya kumkataza mtu mwenye hedhi, nifasi pamoja na janaba kugusa pamoja na kusoma Qur-an isipokua baada ya kuifanya dhamiri ((yamassuhu .....)) ni yenye kurejea katika Qur-an na hilo ni kosa katika upande wa lugha lakini jambo lililowazi ambalo wanavyuoni wengi wa tafsiri wameenda kwa kusema hii dhamiri inarudi kwenye ubao wa Lawhul-mahfudh na jawabu ni kuwa dhamiri ilyomo ndani ya aya inarejea katika ubao wa Lawhul-mahfudh na wala sio katika Qur-an, kwa maana ya msahafu hivyo ni sawa na kusema: "Hapana augusae huo ubao wa Lawhul-mahfudh ila waliotakaswa na mabaya pia waliotakaswa hapa ni

Malaika na wala sio Wanaadamu lau kama utachunga maneno jinsi yalivyokuja.

Na lau kama tutakubali kufaa kwake ya kwamba dhamiri hii iliyopo katika aya inarejea katika Qur-an basi tunasema ""Tahir"" ni katika maneno yenye maana nyingi, kwani hutumika kwa maana ya Muumini, na pia kwa mwenye tohara ya hadathi kubwa, na pia juu ya tohara ya hadathi ndogo, na juu ya yule ambae hakuna katika mwili wake najis, kwahivyo aya hii haioneshi dalili juu ya uharamu wa kugusa na kusoma Qur-an.

Vile vile tunasema inajuzu kwa mwanamme na mwanamke kusoma, kugusa Qur-an, kushika msahafu pasi na udhu, hii ni kwasababu hapana dalili yenye kukataza jambo hilo. Na katika dalili ya hilo hadithi ya Aisha ambapo Mtume { Swallallahu a'layhi wasallam} alikuwa akimtaja Allah katika hali zote, ametoa Imamu Bukhari kwahivyo haijuzu kwetu kumtia dhiki mwanamke katika mzunguko wake wa ibada ambazo aliekewa katika sharia, pia hadithi ya Bibi Aisha (R.A) pale ambapo alipokuwa Hujaji pamoja na Mtume {Swallallahu a'layhi wasallam} na wakateremka katika sehemu iitwayo [sarija] karibu na Makka na Mtume akamkuta (Bibi Aisha) analia kwa hedhi yake, akamwambia "Fanya kila anachokifanya hujaji isipokua usitufu nyumba (alkaba)" hivyo hakumzuwia kusima Qur-an na wala kuingia katika msikiti mtukufu. Hii dalili tosha ya kuwa Mwanamke mwenye Hedhi na Nifasi wanaruhusiwa kusoma, kushika, kugusa msahafu na kusoma Qur-an pia angalia kitabu cha Linnisai

b. Ama kwa upande wa hadithi ambayo wameitolea hoja ni dhaifu haifai kutolea hoja. Angalia sahihi Fiqhi sunnah Juz 1 uk {145}. Katika hadithi hii kuna wasimulizi wake wanakhitilafu kubwa. Sheikh Albani amesahihisha kwa kujumuisha njia zake na akalifasiri neno ""Tahir"" kwa kusema "ni Muumini ni sawa akiwa na hadathi

kubwa au ndogo kwani haijapatikana dalili iliyowazi na iliyosahihi kutojuzu kushika msahafu kwa mwenye hadathi kubwa na ndogo". Angalia Arwail khalili Juz 1 uk 158. Hapana hadithi yoyote ilyo marfuu mpaka kwa Mtume katika kuzuia kusoma na yote yaliyokuja, ni dhaifu hayasimami katika kutolea hoja. Na kauli hii ndiyo madhehebu ya Ibnu Abbas katika masahaba na Said bun Musayyid katika matabiina na Imam Malik na kundi la watu wa kishafi, kwasababu jambo hilo la mwenye hedhi linarefuka muda wake, hivyo itajuzu kwake kusoma Qur-an katika hali hiyo na wala hakuna dalili inayomzuwia kusoma kwake Qur-an, amesema Sheikh Islam "Hakuna katika jambo la kumzuwia mwenye hedhi kusoma" dalili zozote zilizo wazi na sahihi. Hivyo basi yeye anahaki ya kusoma Qur-an kwa haya yafuatayo:-

- Kwamba asili ni kuwa halali mpaka isimame dalili ya kuzuwia.
- Ya kwamba Allah ameamrisha kusoma Qur-an kiujumla na akawasifu wale wenye kukisoma kitabu chake na atakayemtoa mtu yeyote katika waja wa Allah kuisoma Qur-an basi sisi tutamtaka yeye dalili, na ikiwa hakuna dalili sahihi zilizowazi juu ya kuzuwia kwani naye mwanamke ameamrishwa kusoma. Hivyo na mwenye Nifasi ni katika mlango ulio bora kuruhusiwa kwani muda wao (wake) ni mrefu zaidi kuliko wa mwenye hedhi.
  Na alivyokwenda nayo Sheikh Ismail ni madhehebu yenye nguvu……(Ibnu-Taymiyyah).

TANBIHI:

Hatupingi kuwepo kauli nyengine kwa wanazuoni bali sisi tunachukua yenye nguvu na yenye dalili na iliyo sahihi zaidi.

❖ KUINGIA MSIKITINI

Wamekwenda jamhuri ya watu wenye elimu katika maimamu wanne na wasiokua wao juu ya uharamu wa kukaa kwenye hedhi, nifasi na janaba msikitini. Na wameegemea juu ya hao kwa dalili zifuatazo:-

1. Kauli yake Allah ("Enyi ambao mmeamini msikaribie Sala hali ya kuwa mmelewa mpaka mjue mnachokisema na wala wenye janaba ila kwa kukatisha njia mpaka mkoge…..) Qur-an (4:43) wakasema makusudio ya sala hapa ni sehemu za sala nayo ni Msikitini, hivyo katika aya hii kuna kuzuwiya mwenye janaba kuingia kwake msikitini ila awe ni msafiri, kisha wakamkisia mwenye Hedhi na Nifasi kama mwenye janaba.

Jawabu juu ya hoja zao hizo: Tunasema hiyo ni moja kati ya tafsiri za Salaf {wema waliopita} kwa maana ya hii aya, na tafsiri nyengine kwamba makusudio ya sala ni ile sala yenyewe na wala sio msikiti basi itakuwa maana "na wala msikaribie sala mkiwa na janaba ila baada ya kukoga, ila katika hali ya safari basi salini kwa kutayammam na kwa ajili hiyo alisema Allah baada yake "na ikiwa ni mgonjwa au msafiri na hamkupata maji basi fanyeni tayammam". Kisha kwa kule kukisia mwenye hedhi kwa mwenye janaba kwa mtazamo huu ni batili kwani mwenye hedhi amepewa udhuru na wala haimiliki nafsi yake kuondosha hedhi yake tofauti na mwenye janaba yeye ameweza tu kukoga.

2. Hadithi ya Jasrat bint Dajajat kutoka kwa Aisha kwamba Mtume {Swallallahu a'layhi wasallam} amesema "Hakika mimi siuhalalishi msikiti kwa mwenye janaba" ameitoa Abuu Daudi {232} pia baihaqiy Juz 2 uk {442}. Jawabu ni kuwa Hadithi hii ni dhaifu haifai kutolea hoja. Kama alivyodhoofisha Imamu Albani katika dhaifu Abuu Daudi.

3. Hadithi ya Ummu A'ttiyyah kwamba Mtume {Swallallahu a'layhi wasallam} ameamrisha kutolewa vigori…….na mwenye hedhi katika sala ya Iddi ili wapate kushuhudia kheri na maombi ya waumini na wajitenge wenye hedhi na Musala (sehemu ya kusalia). Wakasema basi itapokua kujitenga ni katika jambo la musala wa Iddi basi huko msikitini ni bora zaidi kuzuiliwa.
   Tunajibu kama ifuatavyo:-
   Makusudio ya musala katika hadithi ni sala, kwa kuwa Mtume {Swallallahu a'layhi wasallam} na masahaba zake walikuwa wanasali iddi katika uwanja sio msikitini, na ardhi yote ni msikiti na wala haijuzu kuhusisha katika kuzuwia baadhi ya misikiti pasi na nyengine.
   Hivyo tunasema zipo hoja nyingi za wale wapingao na zote zikajibiwa na wanavyuoni wanaojuzisha, hivyo tunalifananisha hili na la usomaji wa
   Qur-an namna wanavyuoni walivyoelezea kwa hivyo jambo lenye kudhihiri ni kuwa dalili za wenye kuzuwia hazifikii katika darja ya kukata koja kwa moja juu ya kumzuwia mwenye Hedhi mwenye Janaba na mwenye Nifasi kuingia msikitini. Kiufupi ni kwamba mwanamke anaruhusiwa kuingia msikitini, kusoma Qur-an, kushika msahafu na atakaepinga ni juu yake atuletee dalili za wazi wazi juu ya suala hili.

❖ KUSUJUDU ANAPOSIKIA AYA YA SIJIDA {{ SIJIDA TILAWA}}

Na wala hapana kizuwizi kinachoweza kumzuwia kusujudu mwanamke atapokua anataka kusujudu hali ya kuwa ni mwenye Hedhi pindi akisikia aya ya sijida au kama itakua yeye mwenyewe ndie msomaji kwasababu sijida sio sala na wala hapajaekwa masharti juu ya tohara, kwani pamethibiti katika sahihi Bukhari

hadithi No. 4862 " Hakika Mtume { Swallallahu a'layhi wasallam} alisoma suratu Nnajmi akasujudu ndani yake na wakasujudu pamoja na yeye wailamu na washirikina na majini na watu" kwahivyo haiwezekani kusema hakika wote walikuwa wana udhu, pia angalia Jamii Ahkamul Nisaai Juz 1 uk {174}.

❖ KUSHUHUDIA IDDI MBILI

Na hili hakuna ubaya,bali inasuniwa kwa mwenye hedhi kutoka na kushuhudia iddi lakini wajitenge na sala. Suali: Je! Akasahau nay eye au wao wakasali pasi na kujua kama wao wapo kwenye hedhi? Jawabu: Hawatopata dhambi kwa kusahau kwao na wala hawatopata thawabu kwa kusahau kwao kwasababu masharti ya sala hayakukamilika, wanasema wanavyuoni wa Usulifiqhi (ikiwa imeondoka sharti na kilichoekewa sharti kimeondoka)

﴿ والله أعلم﴾

❖ KULALA MWENYE HEDHI PAMOJA NA MUMEWE KATIKA SHUKA MOJA

Kutoka kwa Ummu Salama amesema wakati mimi niko pamoja na Mtume
{ Swallallahu a'layhi wasallam} nimelala katika shuka nikapatwa na hedhi, nikajitenga nae nikachukua nguo za hedhi yangu, akasema: "umetokwa na damu?" Nikasema "ndio" akanita nikalale nae katika nguo moja. Ameitoa Bukhari {298}, Muslim {296}, amesema Imamu Nawawy katika sherhe Muslim Juz 1 uk {954} ""Ndani ya hadithi hii kuna kujuzu kulala pamoja na mwenye hedhi …….. katika nguo moja""

NIFASI

Ni damu inayomtoka mwanamke kwasababu ya uzazi, wamesema baadhi ya wanavyuoni hakika nifasi ila wakati wa uzazi au baada yake na kile anachokiona mwanamke kabla ya uzazi pamoja na uchungu kitakuwa ni hedhi. Na katika hali hii ni juu yake kufanya mambo yote yanayostahiki kufanywa.

Jee! Kila anaezaa anaingia katika nifasi?

a. Kuzaa kunakozingatiwa katika sharia ni kila kilichotimia miezi 4 na ikamtokea damu, hii ni nifasi kwani tayari ishapulizwa roho na kwayakini ameshakua kiumbe.
b. Kuzaa kuharibika mtoto ambapo kunaitwa kuanguka, baadhi ya wanavyuoni wamesema si nifasi ambayo ndio kauli iliyomashuhuri katika madhehebu ya Ahmad bin Hambal. Na baadhi wakasema ni Nifasi kawni Yule aliyeharibu kwanza alikuwa kiumbe na kurejea katika asili ya udamu na mwanamke akatokwa na damu.
   Kiujumla tunasema mimba itapofika siku tisini tayari itakua ni kimbe kilichopo tumboni, basi hivyo ni nifasi na zaidi ya siku tisini kunatilika mkazo zaidi kuwa ni nifasi na mwanaadamu aliyezaliwa kabla ya siku tisini itahitaji uthibitisho.

Na atakapo toka damu ya nifasi mwanamke huenda asione damu na hili ni mara chache sana, na juu ya hili atakaa mwanamke muda wa nifasi, ikiwa atazaa baada ya kuchomoza jua na adhuhuri ikaingia na wala hakuona damu kwa hakika hatakoga bali atatawadha na kusali na kama ataona damu siku 1 au 2 au 10 au 20 au 30 au 4, hiyo itakua ni Nifasi.

WAKATI WAKE

Hakuna mpaka katika uchache wa muda wa nifasi.
Wamekubaliana wanavyuoni juu ya kwamba pindi atakapoona tohara hata kabla ya siku arobaini, atakoga na atasali na atafanya tendo la jimai. Ama ukubwa au urefu wa muda wake, wanazuoni wengi wamesema ni siku arobaini tu. Mwenye nifasi ni kama mwenye hedhi katika hukmu zote za kisheria katika damu, yaliyokua ya halali na yaliyokua yaharamu na yaliyokua Mustahabbu kwake yaani yanayopendezeshwa.
Na Allah ndie ajuae zaidi juu ya haya yote tuliyoyaeleza. Kwani kila sifa njema au shukurani kwa neema zake hutimia mambo mema.

﴿ واالله أعلم﴾

HUKMU YA HEDHI NA NIFASI



NA

YANAYOFUNGAMANA NAYO KATIKA HUKMU ZA KISHERIA

MASJID AL-FAROUQ
MKELE ZANZIBAR